

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



OFISI YA RAIS,
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA JIJI LA DAR ES SALAAM



Tarehe: 24 Agosti, 2020

TAARIFA KWA UMMA


HALMASHAURI YA JIJI DAR YAANZISHA VITUO VYA KUENDELEZA UTAMADUNI, UTALII WA NDANI

Ikiwa katika utekelezaji wa mipango yake ya kuendeleza utamaduni na utalii wa ndani, Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam imeanzisha vituo rasmi vitakavyokuwa vikitoa huduma ya vyakula vya asili kutoka katika mikoa mbalimbali ya Tanzania, sehemu maalumu kwa ajili ya mapumziko na kumbi kwa ajili ya sherehe na mikutano mbalimbali.

Mkurugenzi wa Jiji la Dar es Salaam, Sipora Liana, amesema lengo la Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam ni kuimarisha utamaduni wa Tanzania kwa kuhamasisha wananchi kutumia vyakula vya asili vinavyotumika katika mikoa mbalimbali nchini. **“Tumeanzisha kituo kinachoitwa Forodhani kama kule Zanzibar kitakachotoa huduma ya vyakula vya asili kwa wananchi na watalii wa ndani na nje ya nchi, lengo likiwa ni kuimarisha utamaduni wa Mtanzania, kukuza utalii, kuliiongezea Jiji mapato na kuwawezesha wananchi kupata sehemu ya kupumzika. Kituo hicho tunakiita Forodhani in Dar”**, anaeleza Mkurugenzi wa Jiji la Dar es Salaam.

“Forodhani in Dar” kimeanzishwa katika eneo la Barabara ya Barrack Obama jirani na Hospitali ya Aghakan na Bahari ya Hindi Jijini Dar es Salaam kikiwa na miundombinu yote muhimu itakayowawezesha wananchi na watalii kufurahia maisha katika Jiji la Dar es Salaam. Wafanyabiashara watakaohudumia katika eneo hilo wengi wao ni wajasiriamali hususan wanawake na vijana wanaopata mikopo inayotokana na asilimia 10 ya mapato ya ndani ya Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam ambao wanapewa kipaumbele kikubwa kwa ajili ya kuwajengea uwezo wa kurejesha mikopo yao.

Katika eneo la soko la Karume jirani na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam pia imeanzisha kituo cha michezo ya watoto ikiwa ni pamoja na michezo ya ngumi, bustani ya kisasa kwa ajili ya wananchi kupumzika, kumbi za mikutano, sherehe mbalimbali, maegesho ya magari, maduka ya bidhaa mbalimbali na huduma za vyoo. **“Tunaendelea kutekeleza mipango hii ili kuwavutia watalii na kutoa huduma ambazo wananchi wanazikosa sehemu nyingine,”** anasisitiza, Sipora Liana, ambaye anasimamia kuona kuwa eneo hilo linaloitwa DCC Park (Dar es Salaam City Council Park) maarufu kwa jina la Drimp linatumika pia kutoa burudani ya ngoma za asili kutoka sehemu mbalimbali za nchi kama ilivyopangwa na Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam.


Gaston L. Makwembe

MKUU WA KITENGO CHA ITIFAKI NA UHUSIANO.